




Kitengo cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya
Habari ya Hizb ut Tahrir cha Zindua Kampeni:




KOMESHA VITISHO KWA WANAWAKE WACHA MUNGU WA KIISLAMU WA **KYRGYZSTAN!**



#WAACHENIHURUWANAWAKEWAKIISLAMUKYRGYZSTAN



Mnamo 27 Juni 2020 M, Kamati ya Usalama wa Kitaifa ya Dola nchini Kyrgyzstan iliwakamata **wanawake wa Kiislamu 8 wasiokuwa na tishio lolote** katika mji wa Naryn kwa kushukiwa kuwemo ndani ya Hizb ut Tahrir, chama cha Kisiasa cha Kiislamu kinachofanya kazi kusimamisha serikali ya Kiislamu - Khilafah kwa njia ya Utume. Serikali ya Kyrgyzstan imekipiga marufuku chama hiki kwa madai ya kipuuzi kuwa ni shirika lenye misimamo mikali, licha ya kuwa hakijajihusisha na kitendo chochote cha ghasia, wala kusaidia kisa cha ugaidi tangu kuasisiwa kwake. Wengi wa wanawake walio kamatwa ni kina mama walio na watoto wadogo au walio na jukumu la uchunzaji wazazi wao wakongwe. Mmoja wa wanawake hawa, **Mamirkanova Amangul** alihojiwa kwa masaa mengi huku akimfanyia uangalizi mtoto wake wa kiume aliyefikia umri wa miaka 4 aliyesibiwa na maradhi ya 'Down Syndrome' na ambaye hivikaribuni alikuwa amefanyiwa upasuaji wa moyo. Mwanamke mwengine, Ajumudinova Almagul, alikuwa anampa uangalizi mjukuu wake aliyesibiwa na maradhi ya kupooza kwa ubongo. Kutokana na natija ya kuwekwa kwake kizuizini, mjukuu wake aliangushwa na kifafa. Wakati wa uvamizi wa nyumba **Arunova Erkingul** ambamo idadi kadhaa ya dada zetu hawa wa Kiislamu walikuwa wamekusanyika, madaftari yalipandikizwa yenyе maandishi na maelezo ambayo hayhusiani kamwe na yeyote katika wanawake hao waliokamatwa. Vikosi hivyo vya usalama viliwapekua dada zetu hawa wa Kiislamu kwa njia ya aibu na ya kudhalilisha na kuwaweka katika baridi na njaa kwa kati ya masaa 6 hadi 12 katika kituo cha kizuizi. Na huko, afya ya **Baktybek kyz Mahabat**, ilidhoofika na akapelekwa hospitali. Wawili kati ya wanawake walio kamatwa wanaendelea kufungwa - **Arunova Erkingul** ambaye ni mchunzaji wa mamake ambaye alipata kiharusi na yuko katika hali mbaya, na **Baktybek kyz Mahabat** ambaye ana tatizo la kiafya linalo hitaji matibabu ya mara kwa mara na ni mama wa watoto wawili walio katika chekechea. Watabaki kifungoni hadi uchunguzi ukamilike na hawaja ruhusiwa kuonana na jamaa zao. Endapo watapatikana na hatia ya mashtaka ya serikali, huenda wakakumbwa na miaka kadhaa gerezani..



KOMESHA VITISHO
KWA WANAWAKE WACHA
MUNGU WA KIISLAMU WA
KYRGYZSTAN!



Ukamataji huu ni sehemu ya vita ambavyo **serikali hii ya kitaifa ya kisekula ya Kyrgyzstan** imevizindua dhidi ya Uislamu chini ya pazia hadaifu nayo ni kupambana na ugaidi na kutii maagizo ya mabwana zake wa serikali za Urusi na za Kimagharibi. Katika jaribio lake la kutapatapa la kuupiga vita mwamko wa Uislamu ndani ya nchi yake na kusimamishwa tena kwa utawala wa Mwenyezi Mungu (swt), **Khilafah**, serikali ya Kyrgyzstan imekimbilia kuchafua sura ya da'wah ya Kiislamu na kuwatishia wanawake wa Kiislamu wasiokuwa na hatia na wenyewe kuheshimika ili kuchochea hofu katika kuipigia debe Dini ya Mwenyezi Mungu (swt).

Enyi Waislamu! Msiruhusu uhalifu dhidi ya wanawake wachaMungu wa Kiislamu wa Kyrgyzstan kuendelea bila ya upinzani au kufichika ulimwenguni! Tunawalingania kuunga mkono kampeni hii muhimu kulingania kuachiliwa huru mara moja wanawake hawa wa Kiislamu wasio na hatia kutoka kwa seli za Kyrgyzstan na kukomesha mateso na vitisho vinavyo endelea vya serikali ya kidhalimu ya Kyrgyzstan kwa mabinti waheshimika wa Ummah wa Kiislamu! Mtume (saw) amesema, "**Muislamu ni ndugu yake Muislamu: hamdhulumu, wala hamtelekezi.**"

Fuatilia kampeni hii katika:

www.hizb-ut-tahrir.info/sw/index.php/kampani/1038.html
na
www.facebook.com/womenscmoht

#WAACHENIHURUWANAWAKEWAKIISLAMUKYRGYZSTAN